**12 JUNI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Arobaini na Sita – Tarehe 12 Juni, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabuge, tunaanza na maswali Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

Na. 580

### Ujira kwa maderva wa magari ya IT

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itashughulikia kuboresha ujira wa madereva wa magari ya IT?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua mchango wa sekta mbalimbali katika uchumi ikiwemo sekta ya usafirishaji, tayari imepanga kima cha chini cha mshahara kilichoboreshwa ambacho kimeanza kutumika tarehe 1 Januari, 2023. Hivyo mishahara na maslahi kwa madereva imeboreshwa kupitia amri ya kima cha chini cha mshahara kipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kazi kwa madereva wanaoendesha magari ya *IT* unafanyika kwa kuingia makubaliano ya kazi kati ya mmiliki wa gari na dereva husika ambapo malipo hufanyika baada ya mhusika kufikisha gari linapokwenda. Kwa muktadha huo, mahusiano yaliyopo si ya ajira bali ni makubaliano/mikataba binafsi ya kibiashara *(independent contractor)* kwa ajili ya *contract for service*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, natoa rai kwa madereva wa magari ya *IT* kuingia mikataba ya kazi ya kibiashara na pale ambapo atatokea mwajiri au kampuni ambayo itaajiri madereva kwa ajili ya kuendesha magari ya *IT* atapaswa kuzingatia Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ambayo inaelekeza ulipaji wa ujira kulingana na sekta hiyo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Serikali ndiyo msimamizi mkuu wa mwananchi wa kawaida, hauoni kwamba kuna haja sasa ya Serikali kutoa tamko kwa wamiliki wa magari haya ya *IT* kwa kuwa wao wanapoingia mikataba wanawadhulumu hawa madereva. Sasa Serikali itoe

tamko kuhakikisha wanafuata kile ulichosema cha kima cha chini ili na wao wapate mikataba halali ya kuweza kuendesha magari hayo na kupata ujira unao stahiki badala ya kilometa 900 kulipwa shilingi 100,000? Swali la kwanza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa utaratibu unaonesha deriva wa *IT* aruhusiwi kuwa na msaidizi, tukumbuke kwamba magari haya yanaenda kilomita nyingi sana kwa mfano toka Dar es salaam mpaka Tunduma ni zaidi ya kilometa 900 hakuna haja sasa ya Serikali kuruhusu madereva hawa wawe na wasaidizi ili wapunguze ajali? Kwa sababu mara nyingi magari yao yanadondoka njiani kwa uchovu wa madereva kwa kuwa mtu mmoja peke yake?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hebron Mwakagenda, Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusiana na suala la hawa madereva wa *IT* kuwasimamia na kuratibiwa na Serikali tayari tunayo Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, lakini pia tunayo sheria kwa makubaliano wanayoyafanya mara nyingi wanafanya makubaliano kwa njia ya mdomo. Tumekuwa tukishauri kwa wakati wote kwamba waingie makubaliano kwa maandishi na sababu ya msingi ni kwamba hizo siyo ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu utoaji wa gari ni wa mtu binafsi au kampuni labda anaagiza gari kutoka Japan linapopitia Bandari ya Dar es Salaam kuipeleka nje ya nchi. Kwa hiyo inakuwa ni kazi ya siku moja au ya wakati tu ambapo dereva atakuwa amefikisha gari hiyo kwenye eneo husika, lakini hata hivyo tumekuwa tukizingatia kwamba katika kipindi cha kufanya kazi hiyo azingatie sheria ambayo ya mkataba ambao ni Sura Namba 345 inayo elekeza maslahi ya watu kwanza wanaoingia kwenye mkataba maslahi, lakini pili kuangalia uzito wa kazi

yenyewe husika na ikiongozwa na hili amri ya ajira ambayo ya mishahara hii ambayo tumeitoa ya kima cha chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tutaendelea kusimami hivyo, lakini kwa wale ambao wanafanyakazi kwenye makampuni tumekuwa tukisisitiza wakati wote kuweza kuhakikisha wanakuwa na mikataba ya kazi ili kulinda haki hizo zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili amelieleza kuhusiana na hao madereva wa *IT* kwa nini hawarusiwi kuwa na msaidizi ndani ya gari? Kwenye hili nitalichukua kwa sababu linahusiana pia na Wizara ya Mambo ya Ndani ili kuhakikisha kweli hawa watu wanakuwa na usalama, lakini pia kuongeza usalama kwa watumiaji wa vyombo vya moto katika barabara. Kwa hiyo, talichukua kwa ajili na nanii nishukuru kwamba ni pendekezo zuri tutalizingatia, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Tarimba kwa niaba yake Mheshimiwa Mafuwe.

Na. 581

**Kuongeza kundi la wanaume kwenye mikopo ya Halmashauri**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE K.n.y. MHE. TARIMBA G. ABBAS** aliuliza: -

Je, ni kwa nini Serikali isiongeze kundi la wanaume kwa mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na Halmashauri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEM naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, Mbunge wa Jimbo la Kinondoni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo ya asilimia 10 inatolewa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 Kifungu cha 37A ya mwaka 2018 na Kanuni za Usimamizi na Utoaji wa Mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu za mwaka 2019 na Kanuni za Marekebisho za mwaka 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria hii, mikopo ya asilimia 10 inatolewa kwa ajili ya kuwezesha makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kupata mikopo isiyo na riba kwa kuzingatia kwamba makundi haya hayawezi kupata mikopo katika taasisi zingine za kifedha kwa sababu ya kukosa dhamana na uwezo mdogo wa kumudu riba ili waweze kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kusimamia utoaji wa mikopo hii kwa mujibu wa sheria na kanuni. Aidha, makundi mengine ambayo siyo walengwa wa mikopo hii wanashauriwa kupata mikopo kupitia taasisi zingine za fedha zinazohusika na utoaji wa mikopo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Mheshimiwa Tarimba Abbas, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Serikali iko kwenye maboresho ya utoaji wa hizi asilimia 10; Serikali haioni ni wakati sahihii wa kufanya marekebisho ya sheria pia ili kuongeza kundi la wanaume kwenye utoaji wa mikopo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili; kwa kuzingatia mila, desturi na utamatudini wetu, jamii nyingi ya Tanzania mwanaume ni kiongozi wa familia; hauoni kwa kumuondoa mwanaume kwenye utoaji wa mkopo ni kufanya kumdumisha mwanaume lakini ni ubaguzi unaoondoa umoja wetu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. DEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Tarimba, ambayo yameulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Mafuwe la kwanza juu ya maboresho haya, kwa sasa kama ambovyo amesema mwenyewe Mheshimiwa Mbunge, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI ipo katika mapitio ya sera hii na sheria hii kwa ajili ya kuona ni namna gani inaweza kuboreshwa kuendana na wakati wa sasa na tayari kuna timu ambayo wajumbe wake wameshateuliwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Kairuki na imeishaanza kazi yake na pale itapomaliza kazi yake basi tutaleta kwenye Bunge hili kupitia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya TAMISEMI na baada ya hapo kuileta ndani ya Bunge hili kwa ajili ya kuweza kufanya marekebisho ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la kuwa na wanaume ni namna gani wanaingizwa kwenye unufaikaji wa mikopo hii? Tayari timu hii itaangalia pia uwezokano wa hili lakini katika makundi haya wanaume wapo kwenye makundi ya vijana, wanaume wapo katika makundi ya walemavu lakini tutachukua ushauri wa Mheshimiwa Mafuwe na kuona ni namna gani nao tunaweza tukaangalia wanaingizwaje katika kupata au kunufaika na mikopo hii.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuna Mheshimiwa Neema; Mheshimiwa Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Serikali inaendelea na maboresho na VICOBA ni vikundia ambavyo wananchi ususani wanawake wa Kilimanjaro wameshamiri sana; ni kwa nini VICOBA visiusishwe sasa katika mikopo hii ya asilimia 10?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. DEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokuwa nikisema awali maboresho haya

yanafanyika kwanza ni kutokana na maagizo aliyoyatoa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya kuangalia upya utoaji wa mikopo hii kwa vikundi. Kwa hiyo, naamini katika timu ambayo inafanya kazi watapitia pia hili la VICOBA kuona uwezekano au upi ni urahisi kuweza kuwafikia wananchi wengi zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea. Swali linafuata la Mheshimiwa Minza Mnyika. Mheshimiwa Minza.

Na. 582

**Matengenezo ya barabara mbovu – Simiyu**

**MHE MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE. MINZA S. MJIKA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kwa kutengeneza barabara zote mbovu katika Mkoa wa Simiyu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kisangi, haya umeishauliza swali. Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Minza Mjika, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutengeneza barabara zenye hali mbaya katika Mkoa wa Simiyu kila mwaka kutokana na bajeti inayotengwa. Barabara zenye hali mbaya zimeendelea kupungua kutoka kilometa 1,512.71 sawa na asilimia 36.32 mwaka 2020/2021 hadi kilometa 1,126.38 sawa na asilimia 27.05 mwaka 2022/2023. Hii ni baada ya ongezeko la bajeti kutoka shilingi bilioni 5.13 mwaka 2020/2021 hadi shilingi bilioni 18.38 kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imetenga shilingi bilioni 17.78 kwa ajili ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini katika Mkoa wa Simiyu kufanya ujenzi na matengenezo ya barabara za jumla ya kilometa 995.21 ambazo zitapunguza barabara zilizo na hali mbaya kutoka asilimia 27.05 hadi asilimia 19 ya mtandao unaohudumiwa na *TARURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuzihudumia barabara za Mkoa wa Simiyu kwa kutenga bajeti kwa ajili wa ujenzi na matengenezo ya barabara hizo kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Moja; kwa kuwa changamoto za barabara na za Mkoa wa Simiyu zimekuwa zikiongezeka siku hadi siku, barabara ni mbovu, wananchi wanashindwa kupita na kusafirisha mazao yao; je, Serikali ina mpango gani sasa wa muda mfupi kuhakikisha wanarekebisha barabara za Mkoa wa Simiyu zile ambazo zinachangamoto kubwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa changamoto ya barabara za Mkoa wa Simiyu inafanana na zile za Mkoa wa Dar es Salaam. Mkoa wa Dar es Salaam umekuwa na changamoto kubwa ya barabara chakavu lakini na kukosa mitaro hali ambayo inasababisha wakati wa mvua shuhuli zote za kiuchumi kusimama katika Mkoa wa Dar es Salaam; je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha wanajenga mitaro na kurekebisha ili sasa wakati wa nyakati za mvua magari yaweze kupita? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. DEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza la kwanza hili la mpango wa barabara za Mkoa wa Simiyu kama ambavyo nimeisha kwenye majibu yangu ya msingi, ukiangalia mwaka 2021 Serikali ilikuwa imetenga shilingi bilioni tano kwa Mkoa wa mzima wa Simiyu kwa ajili ya ukarabati wa barabara lakini kuonyesha ni namna gani Serikali inajali wananchi wa Mkoa wa Simiyu, inajali wananchi wake wa Tanzania iliiongezea fedha *TARURA* kutoka shilingi bilioni 226 na kwenda shilingi bilioni 776 zaidi ya mara tatu ya ile bajeti ya mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ukiangalia Mkoa wa Simiyu peke yake kutoka shilingi bilioni tano kwenda shilingi bilioni 17 ambayo imetengwa kwa ajili ya mwaka wa fedha 2023/2024. Hivyo Serikali itaendelea kuweka kipaumbele cha kuhakikisha kwamba barabara zinatengenezwa kwa wakati ili ziweze kupitika na kuendelea kupunguza asilimia ya barabara mbovu kwa kuhakikisha *TARURA* inaendelea kuwekewa fedha kwa ajili ya matengenezo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali la pili kuhusu Mkoa wa Dar es Salaam; wewe pia ni shahidi kwa sababu ni Mbunge wa Mkoa wa Dar es Salaam tayari hivi karibuni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Angellah Kairuki alikaa na Wabunge wote wa Mkoa wa Dar es Salaam na vilevile aliita Kamati ya Bunge ya TAMISEMI na kusaini mikataba kwa ajili ya kuanza Mradi wa *DMDP II* ambayo itakwenda barabara zote ambazo zinachangamoto, zilizosalia ambazo hazikuwepo kwenye *DMDP I* katika Mkoa wa Dar es Salaam ni zaidi ya shilingi bilioni 800 ambayo Serikali hii ya Mama Samia Suluhu Hassan imetenga kwa ajili ya kuhakikisha Mkoa wa Dar es Salaam unaboreka. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mrimi, ajiandae Mheshimiwa Nyongo.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa barabara nyingi za ndani ya Mji wa Mugumu kule Wilayani

Serengeti zina hali mbaya sana na haziwezi kupitika; je, ni lini sasa Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa barabara hizi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. DEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Amsabi Mrimi la lini Serikali itaongeza ukarabati wa barabara zake katika Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilijulishe Bunge lako tukufu kwamba hivi tunavyoongea hivi sasa kuna barabara ambayo inazunguka Soko Kuu la Mji wa Mugumu ambayo inatengenezwa kwa kiwango cha lami kupitia Wakala wetu wa *TARURA* na tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha mazingira ya Mji wa Mugumu kwa sababu ndiyo Makao Makuu ya Wilaya ya Serengeti. Lakini vilevile kupitia Wilaya nzima ya Serengeti barabara za changarawe vilevile tutaendelea kuhakikisha fedha inatengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara zake na nyingine Mheshimiwa Mbunge Mrimi amekuwa akija kwa ajili ya kuzielezea na kusema barabara zipi ziweze kutengewa fedha kwa ajili ya kuzifungua.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nyongo, ajiandae Mheshimiwa Amar na ajiandae Mheshimiwa Mpina.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, majibu ya Serikali ni mazuri sana na Mkoa wa Simiyu umepewa fedha kwa ujumla kama walivyopewa Mikoa mingine. Namuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa umuhimu wa Mkoa wa Simiyu kwa sababu ya zao la pamba, kwa sababu kuna njia mbovu sana kwa mfano sasa hivi tunakwenda kusafirisha mazao ya pamba njia ni mbaya sana kutoka vijijini.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri uko tayari sisi kwa kushirikiana na *TARURA* tulete hesabu ya kipekee kwa ajili ya kupambana na tatizo hili ili muweze kutujengea barabara mbovu katika Mkoa wa Simiyu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. DEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nyongo la kuleta maombi ya kipekee; hivi sasa Serikali kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI imeteua timu ya kufanya mapitio ya namna ya kutoa mgao wa fedha za barabara kwenye Halmashauri zetu kote nchini kwa kuangalia umuhimu wa maeneo, kuangalia masuala ya kilimo yaliyokuwepo hapo, upitwaji wa magari kwa wingi na kadhalika.

Kwa sasa *TARURA* ilirithi mfumo ambao ulikuwa katika *Road Fund* ya namna ya mgawanyo wa fedha hizi zinazopelekwa, lakini baada ya timu hii kumaliza itawasilisha taarifa yake kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na baada ya kuwasilisha taarifa hiyo, watakaa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, pamoja na *TARURA* kuona ni namna gani sasa mgawanyo wa fedha utaendana kutokana na mazingira yaliyoko katika maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwemo kule Jimbo la Maswa anakotoka Mheshimiwa Nyongo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa Mji wa Kharumwa unazidi kupanuka na matengenezo yanafanywa ya mara kwa mara kwenye barabara zetu za mitaa pale Kharumwa, lakini zinaponyesha mvua barabara zile huwa zinaharibika kwa ajili ya ukosefu wa mitaro. Je, Wizara iko tayari kutenga fedha kwa ajili ya kujenga hiyo mitaro ili kunusuru uharibifu wa barabara hizo wakati wa mvua?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TARURA* imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya maboresho ya Mji wa Kharumwa kule Wilayani Nyang'wale anakotoka Mheshimiwa Amar na tutaendelea kuangalia ni namna gani tunapeleka fedha ya kutosha kadri ya upatikanaji

wake, kwa ajili ya kuboresha mazingira ya mji huu hasa ujenzi wa mitaro ambayo upo kule Wilayani Nyang'wale. Nimtoe shaka Mheshimiwa Mbunge, yeye ni shahidi vile vile kwamba *TARURA* imeongezewa fedha zaidi ya mara tatu ya ile iliyokuwepo mwaka wa fedha 2020/2021 na hii ni *commitment* kubwa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Watanzania kwa kutenga fedha ya kutosha kwa *TARURA* kuhakikisha barabara nyingi zaidi zinatengenezwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpina, jiandae Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, Serikali kupitia *TARURA,* Mkoa wa Simiyu iliahidi kujenga Daraja la Mto Sanjo linalounganisha Itilima na Meatu na Daraja la Mto Sanga linalounganisha Maswa na Meatu kwa muda mrefu. Je, ni lini Serikali itatimiza azma yake hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itatimiza azma ya kujenga madaraja haya katika mito hii miwili aliyoitaja Mheshimiwa Mpina, inayounganisha kati ya Wilaya ya Itilima na Wilaya ya Maswa, lakini kuna mingine ambayo ametaja pia ya Wilaya ya Meatu anakotoka yeye Mheshimiwa Mpina. Tutaangalia katika bajeti hii ambayo tunaenda kuitekeleza 2023/2024 na kuona ni kiasi gani kimetengwa na nitakaa na Mheshimiwa Mpina kuweza kuona tunaanza vipi kwa haraka kadri ya fedha iliyotengwa ya ujenzi wa madaraja haya mawili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii. Sehemu kubwa ya Jimbo la Arumeru Mashariki liko kwenye miteremko ya Mlima Meru, kwa hiyo barabara zake kwa mwaka mzima zinakuwa ni mavumbi au mifereji wakati wa mvua. Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga

fedha kwa ajili ya kuzijenga kwa kiwango cha lami au tabaka gumu la namna nyingine kwa teknolojia nyingine yoyote? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Pallangyo la barabara zake hizi za Arumeru Mashariki kwamba, Serikali imeweka *commitment* kubwa kwa kuiongezea fedha *TARURA* kuhakikisha barabara nyingi zaidi zinatengenezwa kwa kuwapa bajeti mara tatu ya ile ambayo Dkt. Samia Suluhu Hassan aliikuta mwaka 2021. Sasa tutakaa na Mheshimiwa Dkt. Pallangyo tutazidi kuangalia ni namna gani *TARURA* inaweza ika-*fast track* utengenezaji wa barabara hizi ambazio wananchi wa Arumeru Mashariki wanazihitaji.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Mwakasaka, kwa niaba Mheshimiwa Kainja.

Na. 583

**Upungufu wa walimu wa shule za msingi vijijini**

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA K.n.y. MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua tatizo la upungufu wa Walimu wa Shule za Msingi katika maeneo ya Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel

Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Jimbo la Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu Mwaka wa Fedha 2018/2019 hadi mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imeajiri jumla ya Walimu 26,598 wakiwemo 16,640 wa Shule za Msingi na 9,958 wa Shule za Sekondari. Kati ya walimu hao, walimu 1,111 walipangiwa kazi Mkoa wa Tabora na kupelekwa kwenye shule mbalimbali. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imeajiri na kuwapangia vituo Walimu 13,130 nchini zikiwemo shule za Mkoa wa Tabora. Kati yao 7,801 ni wa shule za msingi na 5,329 wa shule za sekondari.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kainja.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa majibu mazuri ya Wizara, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza; Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuweka motisha kwa Walimu walioko vijijini, ili tuweze kupata Walimu wengi waweze kwenda kuajiriwa vijijini ili tuweze kuondokana na upungufu maeneo ya vijijini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; Serikali haioni kuna haja ya ajira hizi zinazotoka nyingi zielekezwe vijijini? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza aliyouliza Mheshimiwa Kainja. La kwanza hili la motisha kwa Walimu vijijini, tayari Serikali inalifanya hili kwa kupitia Wakurugenzi wa Halmashauri husika, kuna Halmashauri ambazo Walimu wanaporipoti kazini wamekuwa wakipatiwa magodoro na vifaa vingine vya kuweza kuwapa motisha kubaki katika maeneo yao ya kazi. Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe kule imekuwa ikifanya hivyo na maeneo mengine nchini na tutaendelea kuona ni namna gani tunatoa motisha kwa Walimu hawa wanaoenda

vijijini kadri ya upatikanaji wa fedha na uwezo wa Serikali na bajeti kuruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye swali lake la pili, la haja ya ajira hizi hawa Walimu kwenda vijijini. Walimu hawa wanaajiriwa kutokana na upungufu uliopo kwenye maeneo husika hasa maeneo haya ya vijijini. Sasa naomba nitoe rai hapa kwa Wakurugenzi wa Halmashauri ambao ndio waajiri wa Walimu hawa na wale wa Mkoani Tabora kule anakotoka Mheshimiwa Kainja vile vile, kuhakikisha kwamba hawa wanaopangiwa maeneo haya kwenda kufundisha wanabaki kule kwenye maeneo yale kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni za utumishi wa umma. Kwa sababu Serikali ilifanya *review* ya maeneo yote yenye upungufu wa Walimu na ndiyo maana hawa wanaajiriwa kwenda kuziba mapengo yale yaliyokuwepo kwenye maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kila mmoja akiomba kuhama, ina maana mapengo yale yanazidi kuwepo. Vile vile nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote Serikali itaendelea kuajiri Walimu hawa kwa ajili ya kuziba mapengo haya na upungufu uliopo kadri ya bajeti itakavyoruhusu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso, jiandae Dkt. Mathayo.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika Serikali imeboresha, imejenga shule nyingi za msingi na sekondari na kuna uhaba wa Walimu. Je, Serikali ina mpango gani wa kukidhi mahitaji ya Walimu ambao ni takribani Walimu 1,000 ni pungufu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali mipango yake ya kuhakikisha hakuna upungufu wa Walimu katika Wilaya ya Tanganyika na wilaya zingine hapa nchini, ndio maana imeendelea kuajiri na hivi karibuni ajira 13,130

zimetolewa za Walimu kwa ajili ya kwenda kuziba mapengo na uhitaji uliopo katika maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwemo kule Tanganyika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mathayo, jiandae Mheshimiwa Bupe.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Katika Jimbo la Same Magharibi maeneo ya milimani hasa Kata za Msindo, Mshewa, Vudee, Tae, Suji, Chomi, Muhezi na Ruvu kuna shida kubwa sana ya Walimu na kwa sababu pengine mazingira magumu ya milima. Je, ni lini Serikali itapeleka Walimu wa kutosha katika kata hizo za milimani na kuwapatia motisha? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itapeleka Walimu katika mgao huu wa hawa 13,130, Wilaya ya Same nayo itapata Walimu hawa kwenda kufanya kazi kule na tutaendelea kuajiri kadri ya bajeti itakavyoruhusu kwa ajili ya kuweza kupeleka Walimu kwenye maeneo yote yenye upungufu hapa nchini, ikiwemo kule kwa Dkt. Mathayo, Wilayani Same.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bupe.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, ni lini Serikali itapeleka Walimu wa kike katika shule ya msingi iliyoko Nkasi inaitwa Shule ya Itete na Shule ya Kala?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika ajira hizi mpya 13,130 ambazo Serikali imetoa katika

mwaka huu wa fedha tutaangalia na kuweka kipaumbele katika shule hizi alizozitaja za Itete na Kala kule Wilayani Nkasi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sillo, jiandae Mheshimiwa Hawa.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa mahitaji ya Walimu wa shule za msingi katika Jimbo la Babati Vijijini ni 1,956 na waliopo ni 1,226 na hivyo kuwa na upungufu wa Walimu 730. Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha Walimu wanaopatikana katika shule za msingi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwishasema kwenye majibu yangu ya msingi, Serikali inaendelea kuweka kipaumbele cha kuajiri Walimu na hasa katika shule za msingi kuhakikisha inapeleka Walimu wa kutosha kwenye maeneo yenye upungufu ikiwemo kule Jimboni kwa Mheshimiwa Sillo. Katika hao 13,130 tutaangalia ni mgao kiasi gani ambao Mheshimiwa Sillo amepata kule katika Halmashauri yake na nitakaa naye kumpa hiyo orodha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa. Mheshimiwa Kawawa ajiandae.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Mkoa wa Tabora ni moja kati ya mikoa ambayo shule nyingi sana ziko katika maeneo ya vijijini na hazina Walimu wa kutosha. Je, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kupeleka Walimu maeneo hayo ili kunusuru elimu ya Mkoa wetu wa Tabora?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitoa kipaumbele katika maeneo mbayo

yana upungufu wa walimu ikiwemo Mkoa wa Tabora na ndio maana katika miaka ya fedha iliyopita ikiwemo wa 2021/2022, ukijumlisha wote Mkoa wa Tabora ulipokea Walimu 1,111 na kwa kutambua bado kuna upungufu huo, Serikali ndio maana ilitoa ajira 13,130 kwa kupitia kibali alichokitoa Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan. Kwa sababu Mheshimiwa Rais anapeleka fedha nyingi za ujenzi wa miundombinu ya madarasa naku – *invest* hela nyingi katika elimu hapa nchini, Serikali itaendelea kuweka kipaumbele cha kuajiri Walimu na ikiwemo katika Mkoa ule wa Tabora.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Kawawa, jiandae Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kunipa fursa hii, kwa kuwa Wilaya ya Namtumbo ni wilaya ambayo iko pembezoni kabisa mwa nchi hii Kusini mwa Tanzania mpakani na Msumbiji na ina upungufu mkubwa wa Walimu katika shule zake za msingi. Je, Serikali inaweza ikatupa umuhimu kutugawia Walimu wa kutosha katika shule zetu zenye upungufu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua upungufu uliokuwepo katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo kule Jimboni kwa Mheshimiwa Kawawa na katika ajira hizi mpya 13,130, Wilaya ya Namtumbo nayo itapata mgao wa Walimu wapya kwa ajili ya kwenda kupunguza upungufu uliopo kule wilayani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mnzava, halafu Mheshimiwa Kapinga, halafu Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi hii. Kwa kuwa Halmashauri zote za Mkoa wa Shinyanga hasa vijijini zina upungufu mkubwa wa wafanyakazi. Je, ni nini kauli ya Serikali kutatua tatizo hili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Dkt. Mnzava kwamba, Serikali itaendelea kutatua upungufu wa watumishi wa umma ikiwemo Walimu katika Mkoa wa Shinyanga na mikoa mingine hapa nchini kadri ya bajeti yake itakavyoruhusu na ndio maana katika bajeti ya 2022/2023 Serikali ilitenga ajira 21,000 kwa ajili ya Walimu na kada ya afya, kwa ajili ya kupunguza upungufu uliopo kote nchini ikiwemo kule Shinyanga.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapinga, jiandae Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na mgao huu wa Walimu 13,100 Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ziko shule zilionekana zina upungufu sana wa Walimu, lakini katika mgao huo hazikupata Mwalimu hata mmoja, ikiwemo Shule ya Msingi Litoho. Je, ni lini, sasa Serikali itapeleka Walimu kwenye Shule hii ya Msingi Litoho na shule nyingine za Halmashauri ya Mbinga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upungufu ambao ameuzungumzia Mheshimiwa Kapinga uliokuwepo kule Wilayani Mbinga, Serikali ndio maana imekasimu mamlaka kwa Makatibu Tawala wa Mikoa kufanya msawazo wa Walimu kuhakikisha shule mbalimbali zinapata Walimu kwa kutoa maeneo yenye Walimu wengi zaidi na kuwapeleka kwenye maeneo yenye uhitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi nichukue nafasi hii mbele ya Bunge lako Tukufu, kumwelekeza Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma kuhakikisha kwamba anapeleka Walimu kwa kufanya msawazo ndani ya Mkoa wake katika shule alizozitaja Mheshimiwa Kapinga.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri amesema kwamba mwajiri wa Walimu hawa ni Mkurugenzi wa Halmashauri, lakini Mkurugenzi huyo wa Halmshauri amemnyima nafasi ya kukataa uhamisho wa mtumishi, jambo linalofanya watumishi wengi kuchukua namba tu kwenye hizi wilaya ambazo zipo pembezoni na kuondoka. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha Wakurugenzi wanakuwa na Mamlaka ya kuhamisha kulingana na wanavyoona nafasi inayopatikana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kuchauka. Hili la kukataa uhamisho liko wazi, Waraka wa Katibu Mkuu Utumishi unaeleza wazi kwamba mtumishi wa umma anapoajiriwa atatumikia mwaka mmoja wa *probation* na baada ya mwaka ule anatakiwa kukaa katika kituo chake kipya cha kazi kwa muda usiopungua miaka miwili kabla ya kuomba uhamisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, namna utaratibu ulivyo ni lazima mtumishi anapoomba uhamisho katika barua yake ile awaweke pale KK, Mkuu wake wa Shule, amuweke Afisa Elimu wa Wilaya, amuweke muajiri wake ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri na wale wote wanatakiwa kuweka *comment* pale, kama wanaona kuna uhaba wa watumishi katika maeneo yao, katika barua ile wanavyoandika imepitishwa, aandike kwamba kuna uhaba na huyu nashauri asihame. Barua ile inapofika Ofisi ya Rais, TAMISEMI, wataangalia na zile *comment* za mwajiri na kuzifanyia kazi na kuhakikisha kwamba Mwalimu yule au mtumishi yule hatoki katika maeneo yale ikiwemo kule Liwale. Kwa hiyo naomba Mkurugenzi wa Liwale afuate utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Asya Sharif Omar, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 584

**Uhitaji wa huduma ya kifungua kinywa shule za msingi**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI K.n.y. MHE. ASYA SHARIF OMAR** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa huduma ya kifungua kinywa kwa wanafunzi wa shule za msingi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asya Sharif Omar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa upatikanaji wa huduma ya chakula kwa wanafunzi wanapokuwa shuleni wakati wa masomo katika kupunguza utoro, kuongeza usikivu na kuboresha afya.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu huo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetoa Mwongozo wa Kitaifa wa Huduma ya Chakula na Lishe kwa wanafunzi Elimumsingi unaoelezea taratibu za mifumo ya uchangiaji wa huduma ya chakula shuleni. Aidha, Serikali iliwaelekeza Viongozi wa Mikoa na Halmashauri kusimamia mwongozo wa Lishe wa Mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii, kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kushirikiana na viongozi wa Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ili kuona namna bora ya utekelezaji wa mwongozo wa lishe na kuwawezesha wanafunzi kupata chakula shuleni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Azan Mwinyi.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa vile tayari Serikali imeshatenga bajeti ya kutoa kifungua kinywa katika shule. Je, ni vipi Serikali itaangalia kwa uangalifu zaidi vifungua vinywa hivyo ambavyo vitatolewa katika shule hizo? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza. Kwanza Serikali siyo kwamba imetenga bajeti kwa ajili ya vifungua kinywa, nilichokisema kwenye majibu yangu ya msingi ni kwamba Serikali kupitia Wizara ya Elimu, imetoa mwongozo wa namna gani ya kupata lishe ikiwemo wazazi wa maeneo husika kuchangia katika kupata lishe watoto hawa wakiwa mashuleni.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Dorothy Kilave.

Na. 585

**Hitaji la ofisi za walimu nchini**

**MHE. DOROTHY G. KILAVE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Ofisi za kisasa za Walimu katika kila shule nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dorothy George Kilave, Mbunge wa Jimbo la Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Miradi ya Kuboresha Elimu ya Msingi *(BOOST)* na Sekondari *(SEQUIP)* imeendelea na azma ya kuboresha Sekta ya Elimu Nchini kwa kujenga shule mpya za msingi na sekondari, ambapo hadi sasa shule 231 za sekondari zimeshajengwa na ndani yake kuna majengo ya utawala ambayo ni ofisi za Walimu za kisasa, vivyo hivyo kwa shule za msingi, shule zote mpya ambazo zinaanza kujengwa, hitaji hili limezingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Mradi wa *BOOST* shule nane za zamani zinakarabatiwa sambamba na uboreshaji wa Ofisi za Walimu. Uboreshaji utaendelea kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini je, haioni iko haja ya kufanya nguvu zaidi kwa ajili ya shule hizi za sekondari ambazo ni kongwe hasa katika Jimbo langu la Temeke, Shule ya Kibasila?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; je, Serikali haioni iko haja ya kuongeza pia nguvu katika shule ambazo zilianza kujenga ofisi hizi lakini mpaka sasa hazijaendelezwa mfano kwangu, shule inaitwa Ally Hassan Mwinyi ambayo ni jina kubwa sana. Je, ni lini sasa Serikali itaweza kumalizia ofisi hizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Dororth Kilave, Mbunge wa Temeke, kwanza kuhusu kuongeza jitihada ya Serikali kwa ajili ya kukarabati na kujenga shule hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge na wana-Temeke kwa ujumla kwamba, Serikali hivi karibuni imepeleka shilingi milioni 700 katika Shule ya Sekondari Kibasila kwa ajili ya ujenzi wa mabweni na madarasa, likiwemo

jengo la utawala katika shule ile. Kwa hiyo, ni jitihada kubwa za Serikali hii ya Awamu ya Sita katika kuhakikisha inaboresha miundombinu ya shule za sekondari na shule za msingi katika Halmashauri ya Wilaya ya Temeke na nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye swali la pili kuhusu shule zilizoanza ujenzi wa majengo haya ya utawala zenyewe, ikiwemo shule ya Ali Hassan Mwinyi, nitakaa na Mheshimiwa Mbunge na kuona ni namna gani Serikali inaweka jitihada kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa jengo hili la utawala katika shule hii yenye jina la Rais wetu wa Awamu ya Pili, Mheshimiwa Dkt. Ali Hassan Mwinyi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Kassinge.

Na. 586

**Kutunga Sera ya Ugatuaji Madaraka**

**MHE. ALLY M. KASSINGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatunga Sera ya Ugatuaji wa Madaraka na kutunga sheria ili kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mtaa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha maandalizi ya Rasimu ya Sera ya Taifa ya Ugatuaji wa Madaraka ambapo wadau mbalimbali wameshirikishwa na kutoa maoni yao. Aidha, Rasimu hiyo imewasilishwa katika ngazi ya maamuzi kwa mapitio na maelekezo zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kassinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Pamoja na majibu hayo ya Serikali ambayo yamenipa mashaka katika mawanda ya ushirikishwaji wa wadau, niseme tu kwamba, katika sehemu ambayo Serikali inatakiwa kuwa makini ni katika kutunga sera hii kwa sababu, ndiyo inakwenda kujibu Ibara ya 146 ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Swali la kwanza; Ni kwa kiwango gani wadau katika Mikoa, Wilaya na Halmashauri na kwa upekee wake Waheshimiwa Madiwani wameshirikishwa katika utungaji wa sera hii?

Swali la pili; Je, Serikali iko tayari kutoa *commitment* hapa Bungeni kwamba, katika mchakato huu kabla ya maamuzi sera hii ipitiwe na Wabunge, kama tulivyopitia Sera ya Elimu, kwa lengo la kutoa *input* zaidi na kuboresha utungaji wa sera hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Ally Kassinge, swali lake la kwanza anasema ana mashaka, nimtoe mashaka haya kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ina imani kubwa na Sera nzima ya *D by D* na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, chini ya uongozi wake Mheshimiwa Angellah Kairuki itaendelea kusimamia sera hii ya *D by D* ambayo ni ugatuaji wa madaraka kwenye Halmashauri. Halmashauri hizi ziweze kuwa na uwezo wa kufanya maamuzi yao wenyewe kwa kushirikiana na wataalam ambao wanapelekwa na Serikali katika maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye Sali lake la pili ambalo anataka *commitment*, *commitment* kama nilivyosema hapo nikimjibu swali lake la nyongeza la kwamba, Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, inaamini katika *D-by-D*. Baada ya mwongozo huu kufanyiwa mapitio tutaileta kwenye

Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ili nao waweze kupitishwa kwenye mwongozo ule ambao upo, lakini tutabaki katika *D by D* Mheshimiwa Mbunge na hatutatoka katika hilo kwa ajili ya kuwapa nguvu Waheshimiwa Madiwani kufanya maamuzi yao katika Halmashauri zao.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Venant Protas.

Na. 587

**Chengamoto ya mipaka katika Jimbo la Igalula**

**MHE. VENANT D. PROTAS** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza mgogoro wa mpaka kati ya Wilaya ya Uyui - Tabora katika Kata ya Tura na Wilaya ya Ikungi – Singida?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Venant Daud Protas, Mbunge wa Jimbo la Igalula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Sekretarieti za Mikoa ya Tabora na Singida imeendelea kutatua mgogoro wa mpaka kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Uyui katika Kata za Tura na Wilaya ya Ikungi. Kamati za Ulinzi na Usalama za pande zote mbili zilikwisha kutana. Kila Mkoa ulipewa majukumu kwa ajili ya kutatua mgogoro huo kwa kufanya yafuatayo:

(i) Wataalam wa Wilaya zote mbili kufika uwandani ili kutafsiri ramani, kufuatilia historia ya eneo, kuandaa kikao cha Majadiliano ya Wataalam na kuandaa kikao cha Wakuu wa Mikoa kuelezea yaliyobainika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Wataalam wa Ardhi wa Wilaya ya Ikungi na Wilaya ya Uyui, wanapitia nyaraka mbalimbali yakiwemo matangazo ya Serikali *(GN)* yaliyoainisha Mikoa hiyo, ramani na mihtasari mbalimbali iliyohusika kupima Vijiji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Venant.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kumekuwa na migogoro mingi sana katika maeneo mbalimbali ya Kata kwa Kata, Kijiji kwa Kijiji, Mkoa kwa Mkoa, Wilaya kwa Wilaya. Sasa na wataalam wetu wamekuwa wakisoma hizi ramani kwa muda mrefu sana.

Je, kupitia Wizara yako hauoni kutoa maagizo mahsusi kwa wahusika wakamalize migogoro hii kwa haraka?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili. Kwa kuwa, mgogoro huu mahsusi wa Kata ya Tura na Wilaya ya Singida (Ikungi). Je, hauoni haja ya mimi na wewe Naibu Waziri tukaenda tukaumaliza ili sasa wananchi wabaki na amani na wajue nini wanachotakiwa kuenda na wapi ni mpaka wao? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Venant Protas, Mbunge wa Igalula:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna mgogoro wa muda mrefu katika eneo hili ambalo Mheshimiwa Mbunge amelizungumzia na hasa kuna vijiji viwili vya Makene ambayo ipo katika Kata ya Iyumbu, Wilayani Ikungi na Kijiji cha Nkongwa kilichopo Kata ya Tura, Wilayani Uyui. Tayari jitihada za Serikali kupitia Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya hizi mbili ya Uyui na Ikungi, vilevile Mikoa hii miwili zimekuwa zikifanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nitumie Bunge lako Tukufu hili kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuwaelekeza, Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya wa Wilaya hizi mbili kukutana mara moja wiki hii, kwa ajili ya kupata suluhu ya mgogoro huu na kufanya majadiliano haya yafike mwisho ili mipaka ya Mikoa hii miwili iweze kujulikana na wananchi wajue wanapata huduma kutoka upande gani wa maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, mimi nipo tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge kadri tutakapopata tu taarifa ya Kamati za Ulinzi na Usalama hizi mbili za Wilaya ya Ikungi na Uyui, nitaongozana na Mheshimiwa Mbunge ambae amekuwa mstari wa mbele katika kuwapigania wananchi wake wa Uyui. Nitaongozana nae kwenda kuhakikisha tunafanya mkutano na wananchi hawa na kuwaeleza mipaka iliyopo kwa mujibu wa *GN*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri hongera sana kwa kuelewa vizuri sekta yako. Hongera sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mpina.

Na. 588

**Ukaguzi wa miamala ya uhamishaji wa bei ya mauziano *(transfer pricing)***

**MHE. LUHAGA J. MPINA** aliuliza:-

Je, Serikali imejiimarisha vipi kukagua miamala ya uhamishaji bei ya mauziano ya bidhaa/huduma za makampuni ya Kimataifa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia vihatarishi vilivyopo kwenye miamala husika, Serikali imekua ikichukua hatua mbalimbali zinazolenga kuimarisha udhibiti na kuzuia upotevu wa mapato. Hatua hizo ni pamoja na:-

a) Kuanzisha Kitengo Maalum cha Usimamizi wa Kodi za Kimataifa ndani ya Mamlaka ya Mapato ya Tanzania kuanzia 2011.

b) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa kanuni na miongozo kuhusu ukaguzi wa kodi kwenye kampuni zenye mahusiano.

c) *TRA* imenunua Kanzidata ya *Orbis* kwa ajili ya kupata taarifa za kusaidia kufananisha bei za Miamala ya Kimataifa ili zisaidie kujenga hoja wakati wa ukaguzi unaofanywa kwenye Kampuni za hapa nchini.

d) Tanzania imejiunga na Jukwaa la Kimataifa la Ubadilishaji wa Taarifa za kikodi kwa lengo la kuhakikisha nchi yetu inajenga uwezo wa kubadilishana taarifa za kikodi na nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatarajia kusaini Mkataba ujulikanao kama "*Multilateral Convention on Mutual Administrative Assistance in Tax Matters*" ambao utaiwezesha *TRA*…

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa utulivu, utulivu ndani ya Bunge.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** …utaiwezesha *TRA* kupata taarifa mbalimbali kutoka katika nchi 146 duniani ambazo zitasaidia katika kuongeza ufanisi wa ukaguzi wa Miamala ya Kimataifa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Kwanza niipongeze sana *TRA* kwa hatua walizozichukua kuongeza uwezo wa kukagua hii miamala ya *transfer pricing,* ikiwemo ununuzi wa Kanzidata ya *Orbis* na kuiwezesha Serikali kupata mapato stahiki. Sasa ninayo maswali mawili ya nyongeza:-

Swali la kwanza; hizo hatua ambazo amezizungumza Mheshimiwa Naibu Waziri zimesaidia kwa kiwango gani kuongeza mapato ya Serikali?

Swali la pili; ni kauli gani Serikali inatoa juu ya ongezeko kubwa la taarifa shuku juu ya fedha haramu ambapo miamala ya usafirishaji wa fedha kwa njia ya kielektroniki na fedha taslimu imeongezeka kutoka trilioni 123 hadi trillioni 280 mwaka wa 2023. Sasa ishara hii inaonesha kwamba, kuna ongezeko kubwa la rushwa, ufisadi, *transfer pricing, elicit financial flow, capital flight,* sasa haya matukio haya kwa ongezeko hilo la…

**MHE. NAIBU SPIKA:** Swali Mheshimiwa Mpina, swali.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ongezeko la hizi takwimu Serikali inatoa kauli gani kama *FIU* ilivyotoa taarifa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote kabla ya kujibu maswali naomba kumpongeza Mheshimiwa Mpina pamoja na Wabunge wengine kwa namna wanavyopigania kuona kwamba, ukusanyaji wa mapato unapatikana kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza, kwa kweli, hatua hizi zimesaidia kwa kiasi kikubwa sana. Ndiyo maana inadhihirika hata hivi karibuni tumeona *TRA* wamevunja rekodi katika ukusanyaji wa mapato hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kupitia *TRA* Serikali imeimarisha mifumo ambayo itadhibiti mianya yote ya rushwa na hata njia nyingine za ukwepaji wa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, Serikali kupitia *TRA* imeongeza rasilimali watu kwa kiasi kikubwa sana na hata hivi karibuni nafasi 524 zimetangazwa na mchakato unaendelea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, pamoja na hayo Serikali imekwenda mbali sana, iko sasa hivi kwenye *FATAF (Financial Action Task Force), anti-money laundering, anti-terrorism financing,* Serikali iko vizuri sana. Mimi niko kwenye kikao cha *European Union* na tumeona namna *European Union* wanavyoisifia Serikali ilivyodhibiti utakatishaji pesa na ku-*finance terrorism* katika Taifa letu.

Mheshimiwa *AG*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, nilitaka tu kuongeza ya kwamba, kwa mujibu wa Sheria ya *Anti-Money Laundering,* taarifa shuku zinapowasilishwa kwa *FIU,* baada ya kufanyiwa *analysis* hupelekwa na kufanyiwa kazi na vyombo vyenye dhamana ya kuchunguza na baadae kuchukua hatua za kisheria. Kwa hiyo, taarifa ambazo zimekwishatolewa kwa sasa zinaendelea kufanyiwa kazi na vyombo vyenye dhamana hiyo vilevile. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Suma Fyandomo, kwa niaba yake Mheshimiwa Profesa Manya.

Na. 589

### Vifaa Jengo Jipya la Mama na Mtoto Hospitali ya Meta – Mkoani Mbeya

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA K.n.y. MHE. SUMA I. FYANDOMO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka vifaa kwenye Jengo Jipya la Mama na Mtoto katika Hospitali ya META Mkoani Mbeya?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetoa fedha kiasi cha shilingi bilioni 5.4 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaatiba kwa ajili ya jengo la huduma za Mama na Mtoto katika Hospitali ya Meta, Mkoa wa Mbeya. Aidha, vifaatiba hivyo vimeshaanza kupelekwa na kufungwa katika jengo la Mama na Mtoto kupitia Bohari Dawa *(MSD)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo hili limeanza kutumika na ufungaji wa vifaatiba katika vitengo mbalimbali unaendelea na utakamilika mapema mwezi Julai, 2023. Naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Manya.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika na kuanza kutumika kwa jengo hilo kunaifanya Hospitali ya Kanda ya Mbeya kuongeza uwezo na ufanisi hata hivyo kuongeza pia viatanda kutoka 600 hadi 800.

Je, ni lini Serikali itakapoifanya Hospitali ya Kanda ya Mbeya kupata hadhi ya taasisi kama ilivyo *MOI, JKCI* na nyinginezo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mchakato huo unaendelea wa kuifanya hospitali hiyo kuwa taasisi na bado tunaendelea mjadala, Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha na

Utumishi kuona namna gani tunaweza kufikia hatua hiyo, ili nayo Mbeya iweze kuwa taasisi kama ambavyo hospitali nyingine za Kanda zinakuwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Esther Malleko.

Na. 590

**Mchango wa Serikali katika kuboresha huduma za Hospitali ya KCMC**

**MHE. ESTHER E. MALLEKO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mchango gani katika kuboresha huduma za Hospitali ya KCMC ambayo inatoa huduma za afya kwa Kanda ya Kaskazini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeboresha huduma za Hospitali ya KCMC kwa kupeleka fedha za miradi mbalimbali, kulipia mishahara pamoja na ufadhili wa masomo kwa wataalam kama ifuatavyo:-

(i) Serikali inalipa stahiki na mishahara ya watumishi 905 waliopo KCMC ambapo jumla ya shilingi 983,612,500 hutumika kila mwezi.

(ii) Katika Mwaka wa Fedha 2023 Serikali imepeleka kiasi cha shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya dawa, vitendanishi na vifaatiba.

(iii) Katika mwaka wa fedha 2023 Serikali imetoa fedha kiasi cha shilingi bilioni 5.9 kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa

miundombinu ya hospitali na shilingi milioni 263.6 kwa ajili ya uendeshaji.

(iv) Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetoa ufadhili wa masomo ya ubingwa bobezi kwa watumishi 15 kada ya afya wa *KCMC* wanaosoma ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; je, ni lini Serikali itatekeleza maombi ya kibali cha mabadiliko ya mishahara katika hospitali ya *KCMC* ambacho wameomba tangu mwaka 2011?

Swali la pili; kuna upungufu mkubwa wa wafanyakazi katika Hospitali hii, je, Serikali imejipanga vipi kuweza kutatua changamoto hiyo, ikizingatiwa hospitali hii ni ya Kanda?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa namna anavyoshirikiana na Wabunge wa Mkoa wa Kilimanjaro na namna ambavyo anafanya kazi yake. Swali lake la kwanza kuhusu ni lini Serikali itafanya maombi yale ya kupandisha hadhi na kuongeza mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu swali la kwanza la kuhusu Mbeya Mbeya pamoja na KCMC ni hospitali ambazo ziko kwenye mchakato ambao kuna mjadala kati ya Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha na Utumishi kwa ajili ya kufikia kiwango hicho ambacho Mheshimiwa Mbunge unakitaja. Wiki hii tumepanga tufanye kikao na utumishi ili tuweze kuona ni namna gani tunaweza kujikwamua na kusaidia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ni suala la upungufu wa watumishi. Kama ambavyo nimesema kuna watumishi 905 ambao wanalipiwa na Serikali, lakini wao wenyewe wanalipa kwa mapato yao ya ndani zaidi ya watumishi 400. Maana yake ukiangalia wanao watumishi karibu 1,300 sasa huo upungufu labda tutaenda kuangalia upungufu umetokana na nini. Inawezekana huko nyuma kweli kulikuwa na upungufu unaoletwa na hospitali yetu ya Mawenzi ilikuwa haifanyi vizuri, sasa hospitali yetu ya Mawenzi sasa inafanya vizuri kwa hiyo, wagonjwa wengi watazuiliwa Mawenzi, wataenda wale wanaohitaji kwenda kwenye Hospitali ya Kanda kwa hiyo, huo upungufu unaweza usionekane. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Mheshimiwa Deo Mwanyika.

Na. 591

**Ujenzi wa barabara ya Makambako hadi Njombe**

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ukarabati mkubwa wa barabara kuu ya Makambako - Njombe?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango wa kuifanyia ukarabati barabara yote ya kutoka Makambako – Njombe – Songea yenye urefu wa kilometa 295. Sehemu ya Lutukila – Songea kilometa 95 ipo katika mpango wa ukarabati kupitia Mradi wa *Tanzania Transport Integrated Project (TANTIP)* ambapo Mkataba wa Mkopo nafuu kati ya Serikali na Benki ya Dunia

umesainiwa na zabuni za kumpata Mkandarasi wa ujenzi zinatarajiwa kutangazwa mwezi Juni, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu iliyobaki ya Lutukila – Makambako ikiwemo na sehemu ya Makambako – Njombe urefu wa kilometa 59, Serikali inaendelea kutafuta fedha toka vyanzo mbalimbali vya ndani na nje kwa ajili ya ukarabati. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali. Napenda kusema tunashukuru sana Serikali hata kwa hicho cha kuanza na ukarabati wa barabara kutoka Songea mpaka Lutukila. Hata hivyo ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, barabara hii ni mbaya sana, ni barabara kubwa ya kiuchumi na kuna shughuli nyingi sana sasa hivi. Sasa Serikali, wakati fedha zinatafutwa, hawaoni kwamba kuna umuhimu wa angalau kutenga fedha za kutosha ili maeneo ambayo ni hatarishi kwa magari mengi ya mkaa yaweze kuanza kushughulikiwa kwenye kona kali na miteremko?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Barabara hii ilifanyiwa *redesign* 2012, wakati huo Njombe haikuwa mkoa. Mji wa Njombe ambapo barabara hiyo inapita umebadilika, unakua kwa kasi, umekuwa na *activities* nyingi. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutoa maelekezo kwamba sasa wafanye *redesign* pale katikati ya mji kutoka Kibena mpaka kufika Nundu ili paendane na uhalisia wa Mji wa Njombe ambao unaenda kuwa Manispaa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni utaratibu ambao umezoeleka kwamba katika hizi barabara kubwa, na hasa barabara aliyoitaja ni ya zamani, tumeendelea na tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati maeneo yale yote ambayo yanakuwa yamechakaa sana ili kuhakikisha kwamba wanaosafiri na wasafirishaji hawapati changamoto. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi huo Mheshimiwa Mbunge, Serikali itaendelea kukarabati yale maeneo yote korofi katika hiyo barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, ni kweli kama alivyosema, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Njombe ni mji unaokua sana kama mji na unapitisha magari mengi makubwa. Sisi kama Wizara tunataka tumhakikishie kwamba tutafanya *redesign*. Itakuwa ni *dual carriageway* katika Mji wa Njombe kuanzia Kibena Hospitali hadi Hagafilo na zitakuwa ni njia nne ili kuhakikisha kwamba hakutokei changamoto ya msongamano katika Mji wa Njombe, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Samweli.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kufahamu Serikali imefikia hatua gani katika maandalizi ya kuijenga barabara ya Kondoa – Gisambalang – Nangwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, sijamsikia vizuri barabara aliyoitaja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Samweli, rudia barabara.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kondoa – Gisambalang – Nangwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Barabara ambayo ameitaja kwa kweli mpango mkubwa hasa ni kuhakikisha kwamba kuna daraja kubwa ambalo linaleta changamoto kati ya Kondoa na Hanang. Tunachofanya sasa hivi, kwanza ni kufanya usanifu wa lile daraja, tulijenge, halafu tuimarishe hiyo barabara ili iweze kupitika kipindi chote cha mwaka. Sasa hivi kwa kweli inapotokea masika hiyo barabara haipitiki, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Taska Mbogo.

Na. 592

**Ujenzi wa meli tatu Ziwa Tanganyika**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa meli tatu kwa ajili ya Ziwa Tanganyika kama ilivyoahidi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Kampuni ya Huduma za Meli *(MSCL)* imetenga bajeti katika mwaka wa fedha 2022/2023 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ujenzi wa meli mpya mbili; meli moja ya kubeba mizigo tani 3,500 na meli moja ya kubeba abiria 600 na mizigo tani 400 katika Ziwa Tanganyika. Kwa sasa *MSCL* ipo katika hatua za mwisho za majadiliano na mkandarasi ili kuwezesha kuanza ujenzi wa meli hizo. Mikataba ya ujenzi wa meli hizo inatarajiwa kusainiwa mwishoni mwa Juni, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, jitihada zinafanywa na Serikali za kukarabati Meli ya *MV Liemba.* Kwa sasa Serikali ipo katika hatua za mwisho za majadiliano na mkandarasi kabla ya mkataba wa ukarabati wa Meli ya *MV Liemba* kusainiwa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Taska.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza. Kwanza tunaishukuru Serikali kwa kutenga fedha za ujenzi wa meli mbili kwenye Ziwa Tanganyika, lakini mwaka 2022 Serikali ilitenga fedha, na mwaka huu Serikali imetenga fedha, lakini majadiliano bado yanaendelea: Je, nini mkakati wa Serikali wa kuharakisha ujenzi wa meli hizi mbili?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa wananchi wa Mikoa ya Katavi, Kigoma na Rukwa wanategemea meli za *MV Liemba* na *MV Mwongozo:* Je, lini Serikali itamaliza ukarabati wa meli hizi ili ziweze kufanya kazi kwenye Ziwa Tanganyika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mpaka tunavyoongea hivi tuko kwenye hatua za mwisho kabisa, na wakandarasi wa kuanza kujenga hizo meli kubwa mbili katika Ziwa Tanganyika walishapatikana. Kwa hiyo, wananchi wawe na imani, na ndiyo maana tunategemea kwamba tunaweza hata tukasaini kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha ili tuanze ujenzi wa hizo meli. Mkataba wa ujenzi,

tunategemea watajenga kwa muda wa miaka miwili hizo meli mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali lake la pili, tunatambua kwamba kwa sasa hakuna meli ambayo inafanya kazi katika Ziwa Tanganyika. *MV Liemba* tunavyoongea imeshapata mkandarasi na mkataba ni kwamba ukarabati huo utachukua miezi minane na meli hiyo itakuwa imerudishwa majini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Meli ya Mwongozo, meli hii ina historia yake. Kilichokuwa kimesimamisha hiyo meli isifanye kazi, siyo kwa sababu ya ubovu, ila Serikali ilitaka ijiridhishe kuhusu *stability* ya hiyo meli. Tunavyoongea, tayari Serikali ilishamu-*engage* Mhandisi Mshauri ambaye ni Chuo chetu cha *DMI* kufanya tathmini, na kama kuna marekebisho, yafanyike. Yakishafanyika, hiyo meli pia itarudi majini muda siyo mrefu. Kwa hiyo, tunategemea katika kipindi cha karibuni meli mbili; *MV Liemba* na *MV Mwongozo* zitarudi majini kuanza kufanya kazi katika Ziwa Tanganyika kwa muda wa karibuni sana ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Ghati Chomete.

Na. 593

**Kuboresha Kivuko cha Kinesi**

**MHE. GHATI Z. CHOMETE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaboresha Kivuko cha Kinesi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania *(TEMESA)* inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu (jengo la abiria, ofisi, vyoo na uzio) katika Kituo cha Musoma maarufu kama Mwigobero. Mkandarasi amekabidhiwa eneo la ujenzi kwa ajili ya kuanza kazi. Aidha, ujenzi wa miundombinu upande wa Kinesi umepangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/2024, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chomete.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Kivuko cha *MV Musoma* kilitolewa na Serikali na kivuko kilichopo hakikidhi mahitaji na kina changamoto nyingi sana, kinaweza kusababisha matatizo: Je, ni lini Serikali itarejesha Kivuko kile? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa miundombinu ya ujenzi kule Kinesi inahusisha maeneo waliyokuwa wanamiliki wananchi pale Kinesi: Je, lini Serikali itawalipa fidia wananchi wale ili waweze kupisha mradi huo? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mara, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Kivuko cha *MV Musoma* ambacho kilikuwa kinafanya kati ya Mwigobero na Kinesi kilihamishwa kwenda kutoa huduma katika Kivuko cha Kisorya na Rugezi kwa sababu ya ukubwa wake. Kivuko cha Totuu kilitolewa Chato kwenda Musoma kufanya kazi kwa sababu kituo kilichokuwa kinafanya kazi kati ya Nansio kwa maana ya Kisiwa

cha Ukerewe na Kisorya kilikuwa kimeharibika na kilikuwa kinahitaji matengenezo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kumwambia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba Kivuko cha *MV Ujenzi* ambacho kinafanya kazi kati ya Rugezi na Kisorya tuko kwenye hatua za mwisho kabisa. Kilichokuwa kinafanyika ni kubadilisha *engine,* sasa tunapaka rangi. Tunaamini mwishoni mwa mwezi wa Saba, kivuko hicho kitakuwa kimekamilika ili *MV Musoma* iweze kurudi kwenda kufanya kazi kati ya Mwigobero na Kinesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matengenezo au ujenzi katika eneo la Kinesi, tayari tumeshafanya tathmini na tumeshaainisha wananchi watakaopisha ujenzi wa maegesho. Hivi tunavyoongea sasa hivi, taratibu za kuandaa majedwali ya kuwalipa zinaendelea ili mwakani tunapoanza tuweze kujenga maegesho upande wa Kinesi pamoja na miundombinu yake, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Ujenzi ilitenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa vivuko vipya: Ni lini ujenzi huo wa vivuko vipya utaanza pale Kigamboni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika mwaka huu unaoendelea, Serikali ilitenga fedha za kujenga vivuko vingi, vikiwemo vya maziwa na vya pale Kigamboni alivyovisema Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tunategemea kujenga kivuko kimoja kikubwa, lakini pia kumetokea maombi kadhaa na

Serikali inafanya tathmini kuona baada ya kupata uzoefu wa vivuko hivi vidogo vya Bakhresa, namna ambavyo tunaweza kufanya ni kujenga kivuko kibwa na pia kuwa na vivuko vidogo. Kwa hiyo, kinachoendelea sasa hivi, tuko kwenye taratibu za manunuzi kuhakikisha kwamba kile tulichokipanga tunakifanya pia katika mwaka huu, pamoja na kuongeza vivuko vidogo ambavyo tumeona vinakwenda kwa haraka sana kati ya Kigamboni na Kivukoni, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Mbunda kwa niaba ya Mheshimiwa Kandege.

Na. 594

**Kuboresha utendaji wa Shirika la Mbolea la Taifa**

**MHE. JONAS W. MBUNDA K.n.y. MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani kuboresha utendaji wa Shirika la Mbolea *(TFC)* ili kusambaza pembejeo kwa wakulima kwa wakati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu wa mwaka 2022/2023 Serikali imeunda Bodi ya Wakurugenzi na kuajiri Meneja Mkuu wa Kampuni ya Mbolea Tanzania. Vilevile, Serikali imeipatia *TFC* mtaji wa Shilingi bilioni sita ambao umeiwezesha kununua jumla ya tani 4,500 na kusambaza jumla ya tani 3,851.35 za mbolea kwa wakulima 20,271.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imepanga kuiongezea *TFC* mtaji wa Shilingi bilioni 40 kwa ajili ya kununua na kusambaza pembejeo za kilimo kwa wakulima. Aidha, mpango wa muda mrefu ni kampuni kujenga kiwanda cha kuchanganyia mbolea na eneo la ekari 14.5 limepatikana kwenye Kijiji cha Visegese, Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, Mkoa wa Pwani, ambapo ujenzi utaanza katika mwaka wa fedha wa 2023/2024.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunda.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pia naomba niipongeze Serikali kwa kuchukua jitihada kuhakikisha kwamba shirika hili linafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa shirika hili muda mrefu halijafanya kazi, ni wazi kwamba kuna upungufu mkubwa sana wa wafanyakazi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inaongeza wafanyakazi katika shirika hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kama nilivyosema awali kwamba ni muda mrefu *TFC* haijafanya kazi, ni *obvious* kwamba miundombinu ya maghala ambayo yalikuwa yanatumika kuhifadhia mbolea yana hali mbaya: Serikali imeandaa mpango gani kuhakikisha kwamba maghala haya yanakarabatiwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunda, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la wafanyakazi, ni kweli kampuni hii inahitaji wafanyakazi. Wiki iliyopita, *management* yote ilikuwa hapa kwa ajili ya kwenda kuutetea muundo kwa ajili ya kuanza kuboresha eneo hili na kupata wafanyakazi wapya. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge

kwamba kazi hii inaendelea ya kupata wafanyakazi wengine wa kusaidia kuendesha Kampuni yetu ya *TFC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kuhusu maghala, ni kweli tunayo maghala ambayo yamekuwa na changamoto kwa kiwango kikubwa sana, lakini hivi sasa tunashirikiana na Halmashauri za wilaya husika kwa ajili ya maghala yale ambayo yapo katika maeneo yao tuweze kuyatumia. Pia sisi tunayo maghala yetu ambayo tunayaboresha hivi sasa ili yaanze kufanya kazi hii. Katika fedha ambayo tumeipanga mwaka ujao wa bajeti, pia tumeongeza eneo la kuboresha maghala yetu ili yaweze kutumika vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sangu.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kampuni yetu ya Mbolea ilikopesha wananchi, watu binafsi, vyama vya ushirika na Serikali zaidi ya Shilingi bilioni 18 ambayo ilisababisha kampuni ikawa na mtaji hasi: Je, Serikali ina mpango gani wa kukusanya haya madeni ili kuiongezea nguvu Kampuni yetu ya Mbolea?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la madeni ni kweli na moja kati ya kazi ambazo tumeipa *management* hivi sasa ni kuhakikisha inafuatilia madeni yote na kuhakikisha kwamba madeni haya yanalipwa ili kuongeza mtaji wa Kampuni ya *TFC*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Msimu uliopita wananchi wa Wilaya ya Tarime walipata shida sana kupata mbolea. Walikaa mpaka wiki tatu pale Tarime waking'ang'ania mbolea: Naomba nipate kauli ya Serikali kwamba msimu ujao wa kilimo watu wa Tarime watapata ile shida au itakuwa imeisha? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika msimu uliopita tulikuwa tuna changamoto ya upatikanaji wa mbolea kwa wakati, lakini Serikali imechukua hatua. Tumeshamwelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa *TFRA* na timu yake nzima kuhakikisha kwamba wanaongeza vituo vya mawakala wa uuzaji wa mbolea sambamba na kutumia vyama vya ushirika kama sehemu ya usambazaji wa mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa kuliko yote, nataka niwaondoe hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba mbolea itaanza kuingia nchini mapema mwezi Julai ili wakulima waanze kuinunua mapema kujiandaa na msimu unaokuja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa maswali bado yapo, lakini tuna changamoto ya wageni, ni wengi sana, na kwa vile tutamaliza mapema, naomba niwatangaze wageni wa Mheshimiwa Spika na wageni wa Waheshimiwa Wabunge waliopo ili waweze kutoka, wengine waingie na wao wapate fursa ya kutangazwa vilevile.

Wageni waliopo Jukwaa la Spika ni wageni kutoka Bunge la Namibia, Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge la Namibia ya Usawa wa Jinsia, Maendeleo ya Jamii na Masuala ya Kifamilia; *Honorable Gottard Kasuto,* Mwenyekiti wa Kamati na Kiongozi wa Msafara; *welcome to the Parliament. (Applauses)*

*Honorable Julieta Kavetuna,* Mjumbe wa Kamati; *Honorable Maria Kamutali,* Mjumbe wa Kamati; *Honorable Bertha Dinyando,* Mjumbe wa Kamati; *Honorable Charmaine Tjirare,* Mjumbe wa Kamati; na Ndugu Dorothy Alawi, Katibu wa Kamati, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 32 wa Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, Waziri wa Madini ambao ni viongozi wa Chama cha Walimu Tanzania, Wilaya ya Bukombe, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Geophrey Pinda, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mkurugenzi na Meneja wa Taasisi ya *Geophrey Mizengo Pinda Foundation* kutoka Katavi, karibuni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Deus Sangu na Mheshimiwa Vincent Mbogo ambaye ni Ndugu Karegesa wa Jimbo la Katoliki Sumbawanga. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile ambao ni Wadau wa Kipindi cha Watoto Shangwe kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo pia wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, wakazi wa Kigamboni kutoka Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Aida Khenani kutoka Kata ya Kirando, Wilaya ya Nkansi, Mkoa wa Rukwa. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Rashid Shangazi, Meneja *MWAMCO SACCOS* kutoka Mlalo, Lushoto. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Nicodemas Maganga ambao ni walimu na wajumbe wa CCM Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Pia wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, mwalimu, mzazi na mwanafunzi kutoka Liwale Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

Tunao wageni 62 wa Mheshimiwa Venant Protas ambao ni Waheshimiwa Madiwani wa Kata Viti Maalum na viongozi wa Chama, Wenyeviti, Makatibu Wenezi Kata, Jimbo la Igalula na Viongozi wa Sekretarieti ya CCM. *(Makofi)*

Pia kuna wageni 60 wa Mheshimiwa Dkt. David Mathayo ambao ni Viongozi wa Kata, Wenyeviti, Makatibu Wenezi kutoka Jimbo la Same Magharibi, Mkoani Kilimanjaro. *(Makofi)*

Wageni 43 wa Mheshimiwa Nyamoga, Diwani na Wanakwaya ya Mtakatifu Agustino kutoka Kilolo, Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

Pia wapo wageni 91 wa Mheshimiwa Regina Qwaray ambao ni Viongozi wa UWT Wilaya na Kata, Madiwani kutoka Babati Mkoa wa Manyara. Hao wamekosa nafasi, lakini wakiingia tutawatangaza tena, wapo eeh? Mko huku sawa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni 88 wa Mheshimiwa Jasson Rweikiza ambao ni Wenyeviti Makatibu, Makatibu Wenezi wa CCM kutoka Bukoba Vijijini Mkoa wa Kagera, hao ndio wamekosa nafasi kwa hiyo, wataingia na watatambulishwa. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 100 na walimu tisa kutoka Shule ya Msingi Kilimanjaro ya Jijini Arusha. *(Makofi)*

Kuna wanafunzi 91 na walimu watano kutoka Shule za *Voice Secondary School ya* Jijini Arusha, hao wamekosa nafasi. *(Makofi)*

Pia kuna wanafunzi 94 na walimu nane kutoka Shule ya Msingi Maria De Matias ya Jijini Dodoma hawa nao wamekosa nafasi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge na wageni wetu karibuni Dodoma, lakini niwaombe sasa wote mliotambulishwa mwende sasa wenyeji wenu wakawape chai, wageni wengine waingie. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Wizara ya Maji Mheshimiwa Mwakamo.

Na. 595

**Serikali na wanachi kuendeleza Bonde la Mto Ruvu**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mipango gani ya kuliendeleza Bonde la Mto Ruvu kwa kushirikiana na wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijiji kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza Mpango wa Uhifadhi vidakio vya Maji wa mwaka 2021-2035 ambao unahusisha ushirikishwaji wa wadau mbalimbali ikiwemo wananchi. Kupitia mpango huo, jamii inaelimishwa kuhusu umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji ambapo zimeundwa Jumuiya za Watumia Maji 11 na kupitia Jumuiya hizo, wananchi wanashiriki moja kwa moja kulinda na kutunza rasilimali za maji kwenye maeneo yao. Vilevile, kupitia mpango huo, Bodi ya Maji ya Bonde la Wami Ruvu inaendelea kujenga miundombinu ya kunyweshea mifugo ili isiendelee kunywa maji kwenye vyanzo vya maji hasa mitoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kutafanyika uainishaji wa maeneo ya malisho na vivuko kwa ajili ya mifugo, na kuweka mipango ya pamoja ya matumizi bora ya ardhi hususani kwenye maeneo yanayohusisha vyanzo vya maji. Aidha, katika kuliendeleza Bonde la Wami Ruvu, kazi nyingine zinazotekelezwa kupitia mpango huo ni pamoja na kutambua maeneo ya uhifadhi wa vyanzo, kuyawekea mipaka na kuyatangaza kwenye Gazeti la Serikali kuwa maeneo tengefu ambapo hadi sasa maeneo 230 yametambuliwa, 13 yamewekewa mipaka na mawili yametangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakamo.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niombe kufanya marekebisho kidogo kwa sababu Bonde la Wami Ruvu sio Bonde la Mto Ruvu haya ni mabonde mawili

tofauti lakini pamoja na marekebisho hayo na majibu mazuri ya Serikali juu ya Bonde la Wami Ruvu naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali haioni sasa ni muda sahihi Wizara ya Maji kushirikiana na Wizara ya Mifugo kwenye Jimbo la Kibaha Vijijini kwenye Kata ya Kwala na Dutumi kujenga mabwawa ili kuzuia mifugo isiende kuharibu kingo za Mto Ruvu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa kuna kazi nzuri imefanywa na Serikali kwenye Bonde la Wami Ruvu la kuunda vikundi na kutambua namna wanavyoweza kutoa huduma kwa wafugaji.

Je, Shughuli hizi ambazo zimefanywa kwenye Bonde la Wami Ruvu Serikali haioni sasa ni muda sahihi kuja kuzifanya kwenye Bonde la Mto Ruvu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Michael Mwakamo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote Mheshimiwa Mbunge nakupongeza kwa uelewa, hili ni Bonde la Wami Ruvu lakini unahitaji zaidi tujikite kwenye Bonde la Ruvu na huku kote Bodi yetu ya Maji ya Wami Ruvu inafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na ushirikiano na Wizara ya Kilimo nikutoe hofu sisi ni Serikali tunafanya kazi kwa *team work* kwa hiyo, tutashirikiana na Wizara ya Kilimo kuhakikisha tunaendelea kujenga maeneo ya kunyweshea mifugo maeneo yale kule yenye wafugaji kwa lengo la kuzuia uharibifu kwenye kingo za huu Mto Ruvu na hili tutalifanya kwa umoja wetu kwa kushirikiana kama Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Jumuiya za watumia maji upande wa Ruvu. Tutahakikisha viongozi ambao

wanasimamia Bonde la Wami Ruvu namna walivyofanya upnde huu wamesikia watafanya. Lengo ni kuhakikisha ushirikishwaji wa pamoja unafanyika kwa pande zote.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

Na. 596

**Kupeleka maji ya Ziwa Victoria kwenye vijiji 33 vya Bunda**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza: -

Je, ni lini Mkandarasi wa kupeleka maji ya Ziwa Victoria kwenye Vijiji 33 vya Jimbo la Bunda ataanza kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Boniface Mwita Getere, Mbunge wa Jimbo la Bunda kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeajiri Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kufanya usanifu wa mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda vijiji 33 vya Wilaya ya Bunda utakaokamilika mwezi Julai, 2023. Vilevile, Mtaalam Mshauri huyo ataandaa pia makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kuajiri mkandarasi wa ujenzi atakayeanza kazi katika mwaka wa fedha 2023/2024. Aidha, katika kupunguza adha ya maji kwa wananchi wa Wilaya ya Bunda wakati wakisubiri mradi mkubwa, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali inaendelea kuboresha huduma ya maji Wilayani Bunda kwa kujenga miradi ya maji ya Kiroleri-Kambubu, Mariwanda na Hunyari. Miradi hiyo inatarajia kukamilika mwezi Julai, 2023.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninashukuru kwa majibu ya Serikali. Pamoja na

majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sasa Serikali imetamka wazi kwamba mradi huu utaanza bajeti ijayo 2023/2024 sasa Serikali inaweza kuwaambia wananchi wa Bunda kwamba ni Bajeti kiasi gani imetengwa kwa mradi huo?

Swali la pili; kwa kuwa Serikali imetumia zaidi ya milioni 52 kufanya usanifu yakinifu kama kuchimba malambo ya Salama A, Lakana, Burundu, Kambugu, Tingirima na Mihingo. Je, ni lini miradi hii itakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Boniphace Getere kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na bajeti kwenye Jimbo la Bunda, Mheshimiwa Mbunge unafahamu na nikupongeze kwanza kwa ushirikiano wako ulifika Wizarani umeweza kukutana na Waziri na Katibu Mkuu. Yote hii ni jitihada ya kuona kwamba hili linafanyika. Kwa eneo lako la Bunda zaidi ya bilioni 1.7 imepangwa na itaenda kutumika kutokana na zile bilioni 750 kwenye ule mradi wa Ziwa Victoria kwako ni zaidi ya bilioni 1.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na uchimbaji na ukamilishaji wa haya mabwawa Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Waziri alishakuelekeza vizuri na tumshukuru zaidi Mheshimiwa Rais kwa kutupatia sisi Wizara ya Maji vifaa au vitendea kazi. Tumeshapata mitambo na huu mtambo mmojawapo wa kuchimba mabwawa unaletwa Bunda mahsusi kuhakikisha haya Mabwawa yanakwenda kuchimbwa na yanakamilika na Mheshimiwa Mbunge tutakuharifu tutakwenda pamoja kwa sababu tunashirikiana vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Idd Kassim.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa tayari Mkandarasi anayetekeleza mradi wa Nduku Busangi Ntobo na mradi wa Mwarugulu tayari amesha *supply* vifaa na hajalipwa fedha. Kufanya hivyo, umesababisha mradi kusimama. Ni lini sasa Wizara itaenda kumlipa fedha mkandarasi ili aweze kutekeleza miradi hiyo miwili ya Mwarugulu na mradi wa Busangi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii yote uliyoitaja ni kweli utekelezaji unaendelea na ulipwaji wa madeni kwa wakandarasi tayari tumeanza kama Wizara. Fedha tunavyozipata tunaendelea kupunguza madeni na kuhakikisha wakandarasi wote walipwe ili waweze kuendelea na miradi hii.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Tunaendelea. Mheshimiwa Maige Mbunge wa Tabora kaskazini.

Na. 597

**Hitaji la maji Shule ya Sekondari Ndono – Uyui**

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itachimba visima katika Shule ya Sekondari Ndono Uyui?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Jimbo la Tabora Kaskazini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Serikali ni kuona maji yanapatikana kwa ajili ya matumizi ya jamii, maendeleo ya kiuchumi na mazingira. Shule ya Sekondari Ndono ilikuwa na changamoto ya maji, na katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imepeleka maji shuleni hapo kupitia kisima kilichopo katika Zahanati ya Kijiji cha Ndono na sasa wanafunzi wanapata maji safi na salama. Aidha, Serikali imeanza maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa upanuzi wa bomba la maji kutoka mradi wa Ziwa Victoria kwenda Wilaya za Urambo na Kaliua ambapo wananchi wa Kijiji cha Ndono ikiwemo wanafunzi wa shule ya Sekondari ya Ndono wataongezewa upatijanaji wa huduma ya maji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Almas.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndio majibu bora kabisa ya Serikali, natoa pongezi kwa Mama Samia Suluhu Hassan lakini pia Waziri Aweso na Waziri Prisca Mahundi. Niliomba maji haya kwa ajili ya shule hiyo na nimepewa na wanafunzi pale na jamii yote niipongeze Serikali sana sana, naomba nitoe shukrani zangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali moja tu la nyongeza. Shule hii ina wanafunzi 1500 na ni wengi sana kwa hiyo *bill* ya maji, ankara imekuwa kubwa sana. Je, Serikali inaweza kutoa ruzuku sehemu ya ankara hii ili wote wapate maji, sasa wanafunzi wanachangia maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote nipende kupokea pongezi za Mheshimiwa Mbunge lakini na yeye pia ni kupitia jitihada zake kama mwenyewe anavyosema, alikuja ofsini tuliweza kuongea kwa pamoja na maombi yake tumeyafanyia kazi. Kuhusiana na kuona mradi huu unabaki kuwa endelevu suala la *bill* shuleni na wanafunzi wote waweze kupata maji kila siku, Mheshimiwa Mbunge nimelipokea tutalifanyia kazi kwa pamoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo, Mheshimiwa Condester jiandae.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi. Mtaa wa Mikwambe Kata ya Twaangoma kuna mgogoro wa kisima cha maji ambacho kimejengwa katika kiwanja ambacho amemilikishwa mtu binafsi. Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua mgogoro huo ili wananchi waendelee kupata maji safi na salama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chaurembo kama ifauatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mgogoro huo upo lakini *DAWASA* tayari wanaufanyia kazi na kwa niaba ya Wizara *DAWASA* watahakikisha mgogoro huu unaisha kwasababu maeneo ya aina hii yamekuwa mengi na tumekuwa tukimaliza. Kwa hiyo, hata hili pia sisi kama Wizara tutahakikisha linakamilika ili huu mradi uweze kutoa huduma kwa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Condester.

**MHE. CONDESTER M. SCHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kumekuwa na changamoto ya wanafunzi kwenye Jimbo la Momba kupoteza maisha kwa ajili ya kwenda kufata maji mtoni. Siku za usoni tulipoteza mwanafunzi wa Momba *Secondary* na tukapoteza mwanafunzi wa Sekondari ya Kamsamba kwa sababu wanaenda kufata maji mtoni kwa mwendo mrefu. Je, ni ipi kauli ya Wizara ya Maji kwa udharula wake kwenda kutuchimbia visima kwenye hizi Sekondari ili tusiendelee kupoteza maisha ya watoto wetu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Condester kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikupe pole sana kwa wananchi kupata kadhia hizi lakini sisi kama Wizara ni sehemu ya kuona kwamba tunafikisha maji safi na salama maeneo yote yanayotoa huduma, na kwa eneo hili la shule naomba nikuahidi kwamba tutakuja kuwachimbia kisima na kama kuna kisima jirani basi tutafanya *extension* ili kuhakikisha wanafunzi hawaendi mtoni na kupata madhara.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Nishati Mheshimiwa Maimuna Ahmad.

Na. 598

**Kukatika umeme mara kwa mara – Lindi**

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN** aliuliza:-

Je, ni lini tatizo la kukatika umeme mara kwa mara Mkoani Lindi litakwisha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Lindi unapata umeme kutoka katika vyanzo viwili ambavyo ni mitambo ya kufua umeme wa gesi iliyopo Mtwara na Lindi (Somanga).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi kifupi (siku 90), Serikali imeandaa mkakati wa kuongeza upatikanaji wa umeme mikoa ya Lindi na Mtwara kwa kupeleka jenereta ya megawati 20,

kufanya ukarabati wa miundombinu ya kusambaza umeme na kufunga vifaa vinne vya kuzima na kuwasha umeme (Autoclosers) kwenye njia mchepuko. Utekelezaji wa Mipango hii ulianza mwezi Mei, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati mitatu ya muda mrefu ni kujenga njia yenye msongo wa kilovoti 220 Songea – Tunduma (mradi huu ulianza mwezi Machi, 2023 na utachukua miezi 18). Kujenga njia yenye msongo wa kilovoti 220 Tunduru – Masasi, Mkandarasi atakabidhiwa eneo la mradi mwezi Juni, 2023. Ujenzi wa njia yenye msongo wa kilovoti 220 Masasi - Mahumbika ambayo upembuzi utaanza mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua nyingine kubwa, Serikali inaendelea na mazungumzo na Shirika la Maendeleo la Japan *(JICA)* juu ya ujenzi wa kituo kikubwa kitakachozalisha Megawati 300 Mkoani Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** miradi hii itakapokamilika, hali ya umeme katika mikoa ya Mtwara na Lindi itaimarika sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pathan.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuwapongeza viongozi wa *TANESCO* Mkoa wa Lindi na Kanda ya Kusini, kuna Mkurugenzi wa Kanda Eng. Makota, kuna Meneja wa Mkoa wa Lindi Eng. Kahinda na mameneja wa Wilaya zote Mkoa wa Lindi wamejitahidi sana kubadilisha hali ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha *Grid* ya Taifa inapita katika Wilaya zote za Mkoa wa Lindi na Mtwara ili kuondoa adha hii ya umeme?

Swali la pili, gesi kwa asilimia kubwa inatoka Mkoa wa Lindi na Mtwara lakini wenyeji wa Mkoa wa Lindi na Mtwara mpaka sasa hivi wanatumia kuni na nishati ya mkaa kupikia. Je, Serikali

haioni sasa ni wakati mwafaka wa kuwasaidia kuwapelekea umeme wananchi wale ili tuweze kulinda mazingira ya nchi yetu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa niaba ya Wizara na Serikali kwa ujumla nipokee pongezi kwa ajili ya hawa watendaiji wa *TANESCO* ambao wanafanya kazi nzuri na wanajitahidi kuhakikisha kila eneo kwa kweli huduma ya umeme inakuwa ya kuimarika. Niwaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba sisi Serikalini na wizarani na wenzetu wa *TANESCO* tutaendelea kuhakikisha jambo hili tunalifanyia kazi kwa sababu ndio kazi yetu ambayo mmetuamini nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la pili kwa sababu Mkoa wa Lindi tayari unayo miundombinu ya umeme, tutakapokuwa tumefikisha *Grid* pale Masasi au Tunduru tayari Mikoa yote na Wilaya zote za Mkoa wa Lindi zitakuwa zimepata umeme wa *Grid* ya Taifa. Kitakachoendelea kufanyika ni kuendelea kusambaza umeme kwa kutumia miradi yetu ya *REA* kwenye vijiji na vitongoji ili kila mwananchi sasa aweze kupata umeme. Kwa hiyo, miradi hii mitatu mikubwa niliyoisema itakapokuwa imekamilika na Gridi itakuwa imeingia Mkoa wa Lindi na tayari kila wilaya itapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la pili kama tunavyofahamu sote Serikali imeanza sasa jitihada kubwa sana za kuhakikisha wananchi wote wanatumia nishati safi ya kupikia ambayo ni pamoja na gesi asilia, gesi za viwandani lakini pia na umeme, na katika maeneo yote ya Lindi na Mtwara tutaweka nguvu za ziada na jitihada kuhakikisha, zile nyumba chache ambazo tayari zimeunganishwa na gesi ya asili basi zinaongezeka kutoka kwenye idadi iliyopo kwa miradi ambayo tumeipanga kwenye bajeti inayokuja ili wananchi wengi zaidi waweze kutumia gesi asilia na hii mitungi mingine ya kawaida ya kuweza kupata nishati safi ya kupikia.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Kaboyoka.

Na. 599

**Kufanya tathmini kampuni zilizo chini ya *NARCO***

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itafanya tathmini ya kampuni zilizo chini ya *NARCO* ili kuona tija zake katika uchumi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Ranchi za Taifa *(NARCO)* inamiliki ranchi 15 na imewekeza katika ranchi nane kati ya hizo. Aidha, *NARCO* imegawa vitalu na kukodishwa kwa wafugaji na kampuni binafsi kwa ajili ya ufugaji wa kisasa na wa kibiashara. Mwezi Oktoba, 2022 Serikali kupitia Kampuni ya Ranchi za Taifa *(NARCO)* ilifanya tathmini kwenye vitalu 116 ambavyo vimekodishwa kwa wafugaji ili kubaini hali ya uwekezaji kulingana na mipango ya biashara iliopo kwenye mikataba yao. Katika tathmini hiyo ilibainika kuwa wawekezaji 76 wamewekeza kulingana na mkataba na wawekezaji 40 wameonesha kutofanya vizuri kulingana na mikataba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tathimini ilibaini kuwa *NARCO* inakabiliwa na changamoto za kimtaji, hivyo imeandaa andiko la mabadiliko ili kuiwezesha kupata mtaji kutoka vyanzo mbalimbali vya fedha. Hata hivyo, ili kuimarisha Kampuni ya *NARCO* na kuongeza tija, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imewekeza kiasi cha shilingi bilioni 4.6 kwa ajili ya kununua ng'ombe wazazi, kuchimba visima virefu na kununua mitambo ya kulima, kuvuna na kuhifadhi malisho ya mifugo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kaboyoka.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali ina mpango wa kuendelea kuwapatia vijana wetu ajira; na kwa kuwa tumeona sehemu kubwa ya ranchi bado hazitumiki.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kugawia vijana wetu maeneo ya kufuga na wakawafundisha ufugaji bora ili waweze kuwekeza sawa na wale wenzetu katika sekta ya kilimo walivyofanya? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mpango tulionao sasa hivi ni pamoja na kuongeza maeneo na kugawa maeneo ambayo hayatumiki kwa vijana ambao sisi Wizara ya Mifugo na Uvuvi tumepanga kufanya hivyo katika mwaka wa fedha unaokuja. Kwa hiyo, liko kwenye mpango na tunakwenda kulitekeleza, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunandelea, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Nyamoga kwa niaba yake swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Kabati.

Na. 600

**Hitaji la minara ya simu Kata za Kilolo**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI K.n.y. MHE. JUSTIN L. NYAMOGA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga minara ya simu katika Kata za Masisiwe, Udwekwa na Nyanzwa Wilayani Kilolo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Jimbo la Kilolo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* ilibaini changamoto ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano katika Kata za Udekwa, Nyanzwa na Masisiwe ambapo tayari imekwishawapata watoa huduma wa kufikisha huduma za mawasiliano katika kata za Masisiwe na Nyanzwa wakati Kata ya Udekwa itaingizwa katika orodha ya miradi itakayotekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Wilaya ya Kilolo imekuwa na changamoto nyingi sana na katika Wilaya hiyo hiyo kuna Kata ya Mahenge, Ukwega, Lugalo na Ihimbo wananchi wanapata shida sana ya mawasiliano.

Je, ni lini sasa Serikali itaondoa changamoto hizo ili wananchi wa Kilolo waweze kupata mawasiliano ya uhakika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Thea.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge wa Iringa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Kilolo walileta maeneo takribani 12 ambayo yalikuwa na changamoto ya mawasiliano,

lakini eneo la Ilambo, Itimbo, Lugalo, Udekwa, Ukwega tayari tumeweka minara ya mawasiliano na huduma zinaendela.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kata nyingine ambazo tumezipelekea fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo takribani shilingi bilioni 1.28 imekwishapelekwa kwa ajili ya kujenga minara nane katika Kata saba za Jimbo la Kilolo, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea, halafu Mheshimiwa Zedi.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana; sasa licha ya Serikali kutoa namba ya kuwaripoti matapeli wa mitandaoni, je, Serikali ina mpango gani wa kuona sasa waathirika wanapata mrejesho badala ya kutegemea majibu ya *automatic* yale mifumo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ntara kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze kwa swali zuri ambalo linatarajia kutoa elimu kwa watu wote. Kwanza kabisa, tuna namba 15040 ambapo ukikutanaa na namba za kitapeli basi unaweza ukatuma ujumbe na ujumbe huu utafika *TCRA*, baada ya hapo *TCRA* wataendelea kuufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nipokee ushauri wa Mheshimiwa Mbunge wa kuona ni namna gani baada ya tatizo kufanyiwa kazi basi mtoa malalamiko aweze kupatiwa mrejesho.

Mheshimiwa Spika, tutalifanyia kazi, lakini vilevile napenda kuwaomba watanzania pale ambapo wanapigiwa simu na mtu akajitambulisha kwamba natoka Vodacom, Tigo na kadhalika basi naomba sana wapokee namba ambayo ni huduma kwa wateja ambayo ni namba 100. Tofauti na namba hiyo basi

tuelewe kwamba hao sio watumishi wa *Vodacom, Tigo* wala kampuni yoyote ya mawasiliano, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Zedi, ajiandae Mheshimiwa Grace Tendega.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante; Vijiji vya Nsumba na Mboga, Kata ya Semembela na Kijiji cha Idubula na Burunde, Kata ya Karitu vimekuwa vikiwekwa kwenye mpango wa kujengewa minara kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote lakini karibu miaka miwili sasa inapita na minara haijengwi.

Je, sasa Serikali inatoa kauli gani au *commitment* gani kwamba safari hii vijiji hivi vya Nsumba, Mboga, Idubula na Burunde vitajengewa minara ya simu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zedi, Mbunge wa Bukene kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ina dhamira ya kuhakikisha kwamba utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi inaendelea kutekelezwa kwa kiwango kikubwa. Ni kweli kabisa nchi yetu ina vijiji zaidi ya 12,300; tunakwenda hatua kwa hatua na tayari tunapeleka minara 758, tumefanya tathimini katika vijiji 2,224 lakini vilevile tunakwenda kupeleka minara 600 kwa ajili ya huduma ya mawasiliano katika vijiji vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini kwamba katika awamu ijayo vijiji vya Idubula, Burunde pamoja na vijiji ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja tutaviweka katika hatua hizo za utekelezaji ili wananchi wa Bukene wapate huduma ya mawasiliano bila kuwa na changamoto yoyote.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Grace, ajiandae Mheshimiwa Chumi, Mheshimiwa *Advocate* Olelekaita na Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi; ni lini Serikali itaiongezea nguvu minara ya *TTCL* iliyoko katika Kata ya Maguliwa, Jimbo la Kalenga, Kata ya Wasa na minara ya Airtel ambayo iko Kata ya Ulanda?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama iifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuelewa kuwa kuna haja ya kuongeza nguvu katika minara kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa tuna zaidi ya minara 800 ambayo inahitaji kuongezewa nguvu. Serikali imeanza na awamu ya kwanza ya kuongeza minara 408 na mpaka sasa kwenye mradi wetu wa Tanzania ya Kidigitali ni minara 302 inakwenda kuingizwa katika utekelezaji na kuhakikisha kwamba minara hiyo inapata nguvu ya kutosha na kupata huduma za *internet.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimuombe Mheshimiwa Mbunge awe na subira kidogo wakati Serikali inatafuta fedha ili tuhakikishe kwamba Tanzania yetu yote inakuwa ya kidigitali.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Chumi, ajiandae Mheshimiwa *Advocate* Olelekaita.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, baadhi ya maeneo ya Kata za Rungemba, Bumilayinga na Isalavanu na Kata ya *Sao Hill* hazina mawasiliano ya uhakika.

Je, ni lini Serikali itafunga japo mnara mmoja kuzunguka maeneo hayo ili wananchi hawa wapate mawasiliano ya uhakika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nipokee changamoto ya Mheshimiwa Chumi ili Serikali ikafanyie kazi na pale fedha zitakapopatikana tutafikisha huduma ya mawasiliano, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Advocate* Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru; kwa kuwa kama wateja tumekuwa tunaripoti hao wanaotutapeli kwa makampuni ya simu, lakini hatupati mrejesho.

Nini kauli ya Serikali kwa Makampuni ya Simu ambayo hayatupi mrejesho wa namna gani wana-*deal* na matapeli hawa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Olelekaita, Mbunge wa Kiteto kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie fursa hii katika Bunge lako tukufu kuwaelekeza *TCRA* wakae na watoa huduma wote ili waone njia iliyosahihi zaidi ya kuhakikisha kwamba malalamiko yanayofikishwa basi Watanzania wanastahili kupata mrejesho wa malalamiko yao ili iwe rahisi kuweza kupima utekelezaji unakwenda kwa kipimo gani kulingana na malamiko yanayotumwa na mrejesho unaokuja. Hivyo, namwelekeza Mkurugenzi Mkuu na timu yake yote walifanyie kazi na sisi kama Serikali tutaendelea kufuatilia kwa karibu sana, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Anatropia, jiandae Mheshimiwa Butondo, na ajiandae Mheshimiwa Dkt. Kimei.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ni suala la kawaida kuona sehemu "A" ina mtandao mmoja na sehemu "B" haina mtandao mwingine kwa maana hapa kuna Tigo, hapa kuna Vodacom.

Sasa ningetaka kujua ni utafiti gani ambao umefanyika na kuonesha mnara mmoja hauwezi kutoa mawasiliano ya mtandao zaidi ya mmoja? Moja, tukifanikisha hilo tutaweza kupunguza gharama, lakini pia tutaweza kupunguza madhara yanayotokana na hiyo mitandao au minara kwenye maeneo ya watu.

**NAIBU SPIKA:** Naona huyu ametoa ushauri. Haya Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Kagera kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nitakuwa nimemuelewa vizuri anaongelea *co–location;* kama anaongelea *co-location* tunafanya *cost benefit analysis* ya watoa huduma anapoona kwamba hapa atakwenda kupata faida na pale atakapoona kwamba hawezi kupata faida hatoweza kufika pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana sasa Bunge lako tukufu lilipitisha Sheria Na. 11 ya mwaka 2006 kwa kuanzisha Mfuko wa Mawasiliano kwa wote ili kuhakikisha kwamba Serikali inakwenda kutoa ruzuku na kufikisha huduma ya mawasiliano katika maeneo ambayo hayana mvuto wa kibishara ili Watanzania wote wapate huduma ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa upande mwingine napokea ushauri wake na sisi tutaendelea kufanya utafiti ili kuboresha zaidi huduma ya mawasiliano nchini.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Butondo, Mheshimiwa Kimei na atamalizia Mheshimiwa Maganga.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naipongeza Serikali kwa kunipa kandarasi ya utengenezaji wa minara tisa katika Wilaya yangu ya Kishapu, lakini kuna kata ya Ngofila, Kata ya Bunambiu na Mwasubi haziko kwenye orodha hiyo ya vijiji ambavyo vitakwenda kupata huduma hizo. Nini tamko la Serikali katika maeneo haya kuhakikisha kwamba huduma hiyo inapatikana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Butondo, Mbunge wa Kishapu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimshukuru kwa kuipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumpelekea minara tisa aliyoipata katika kipindi cha miaka miwili. Kwa hiyo, tunaamini kwamba hiyo ni hatua nzuri kabisa ambayo tunatakiwa kuendelea kuishukuru Serikali hii, lakini vilevile hatutakomea hapo na awamu zinazokuja tutajiridhisha na changamoto iliyopo katika kata ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja ili tuziingize katika utekelezaji. Aidha, kama ni kuongeza nguvu ama kupeleka mnara, wataalam wetu watuambia ili kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata huduma ya mawasiliano. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei, jiandae Mheshimiwa Maganga.

**MHE. DKT, CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, je, Serikali itakuwa tayari kuweka wazi mkeka wa mgawanyo wa minara 758 na hiyo mingine 600 tuliyoahidiwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Kimei, Mbunge wa Vunjo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iko tayari. Sisi kama Serikali tupo kwa ajili…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, swali lilikuwa kama mko tayari, ahsante mpo tayari. Mheshimiwa Maganga.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kumuuliza swali Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasilano na Teknolojia ya Habari, unakumbuka mwaka 2021 ulifanya ziara kwenye Jimbo langu ukawaahidi wananchi wa Mbogwe minara mitano, lakini mpaka sasa hivi haujatimiza ahadi yako.

Je, ni lini unakwenda kutekeleza ahadi yako ambayo mimi na wewe tulifanya mkutano kule Mbogwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maganga, Mbunge wa Mbogwe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa nilifanya ziara katika Wilaya na Jimbo la Mbogwe na Serikali iliahidi kufikisha huduma ya mawasiliano, na mwezi wa saba wakandarasi wataingia *field* kwa ajili ya kuanza utekelezaji mara moja, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha, lakini mimi niipongeze Wizara hii na Wizara nyingine kwa kweli mawasiliano yameboreka hongereni sana. *(Makofi)*

Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutoa bajeti ya kuimarisha mawasiliano, lakini tuwapongeze Mawaziri wawili na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri mnazofanya. *(Makofi)*

Wageni waliopo Bungeni muda huu ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Stephen Byabato, Naibu Waziri wa Nishati kutoka Bukoba Mjini, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 91 wa Mheshimiwa Regina Qwaray ambao ni Viongozi wa UWT Wilaya na Kata, Madiwani kutoka Babati Mkoa wa Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 88 wa Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Wenyeviti, Makatibu na Makatibu wenezi wa CCM kutoka Bukoba Vijijini Mkoa wa Kagera. Haya Ndugu Rweikiza tumeona na sisi tutaiga. *(Makofi)*

Pia tunaye mgeni wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani kutoka Jijini Mwanza, karibuni sana. (*Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 91 na walimu watano kutoka *The Voice Secondary School* ya Jijini Arusha, karibuni. *(Makofi)*

Wanafunzi 94 na walimu nane kutoka Shule ya msingi Maria De Matias ya Jijini Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu amemteua Mheshimiwa Simbachawene Kukaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Bunge Serikalini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wote naomba kuwakumbusha kuwa Wizara ya Fedha na Mipango itaendesha semina kuhusu matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi pamoja na Sensa ya Majengo ya mwaka 2022. Semina hii itafanyika leo siku ya Jumatatu tarehe 12 Juni, 2023 mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge katika Ukumbi wa Pius Msekwa. *(Makiofi)*

Waheshimiwa Wabunge wote mkaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu ili kufahamu jinsi ya kutumia matokeo ya sensa hiyo na kufuatilia miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Sasa ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho 3.00 asubuhi.

*(Saa 4.55 Asubuhi Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 13 Juni, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*